SHULE YA SEKONDARI LUGARAWA,
S.L.P  517,
NJOMBE.
***Mob- 0768099803***
0 3/12/2021

Kumb. Na. **LUGSS/F.I/2021/…….**
Jina la mwanafunzi …………………………..
-------------------------------------
S. L. P ---------------
-------------------------------

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA KWANZA  MWAKA 2019**

**1.0 Utangulizi.**

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Kwanza katika shule hii mwaka 2019. Uripoti shuleni tarehe **…………**Shule ya Sekondari LUGARAWA ipo katika kata ya Lugarawa, wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe ukitokea Njombe/Ludewa kuelekea Ludewa/Njombe shuka Mkiu kisha elekee barabara ya kwenda Lugarawa, kutoka Mkiu  umbali ni kilometa 16.

Masomo yataanza rasmi tarehe**11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **07/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** ndani ya siku saba toka tarehe  ya kuanza masomo.

**2.0 Mambo Muhimu ya Kuzingatia.**

**2**.1 **SARE YA SHULE**

**A: MAVAZI YA  DARASANI**

**(i) Wasichana**

- Vigauni viwili (2) vyeupe vyenye malinda chini shingo duara (mshono umeambatanishwa)
- Suruali mbili (2) rangi ya Damu ya Mzee (aina ya Kitambaa imeambatanishwa)
- Tshirt ya bluu shingo duara 1
- Jozi mbili(2) za soksi nyeupe
- Tai rangi ya Damu ya Mzee
- Viatu vyeusi visiwe na kisigino kirefu viwe vya kufunga na kamba vya kupiga kiwi jozi mbili(2) **visiwe vya plastiki (Yebo**)
- Sweta rangi ya bluu nyeusi  (dark blue)

**(ii) Wavulana**

- Suruali mbili(2) rangi ya Damu ya Mzee (Aina ya kitambaa imeambatanishwa)
- Mashati mawili(2) meupe mikono mirefu yenye ukosi (kola) shingoni
- Tshirt ya bluu shingo duara 1
- Jozi mbili (2) za soksi rangi nyeusi
- Tai rangi ya Damu ya Mzee

- Viatu vyeusi jozi mbili (2) visiwe na kisigino kirefu viwe vya kufunga na kamba vya kupiga kiwi, **visiwe "buti, raba wala yebo**"
- Sweta rangi ya kijani

**B: MAVAZI KWA AJILI YA MICHEZO**

**(i) Wasichana**

- Bukta ya rangi ya bluu au traki suti
- Fulana ya njano,
- Raba rangi yoyote

**(ii)Wavulana**

- Bukta ya rangi ya bluu au traki suti
- Fulana ya njano,
- Raba rangi yoyote

**C: VIFAA VYA DARASANI**

- Madaftari 9 (Counter book Quire 3) na za kawaida 3, Kalamu mbili,Peni za bluu au nyeusi za kutosha, mkebe wa hesabu mmoja (1) na vifaa vyake vyote na Rula 1.
- Kibegi cha kubebea madaftari kimoja (1)
- Kamusi ya kiingereza kwa kiingereza na vitabu vingine kama utaweza.

**D: MAVAZI KWA AJILI YA KAZI ZA MIKONO**

**(i) Wasichana**

- Suruali rangi ya zambarau
- Fulana ya njano
- Raba rangi yoyote

**(ii)Wavulana**

- Suruali rangi nyeusi
- Fulana ya njano
- Raba rangi yoyote

E. FEDHA NA **VIFAA VYA KAZI ZA MIKONO**

- WASICHANA – Jembe jipya lenye mpini na ufagio wa chelewa
- WAVULANA - Kindoo cha lita 10 kimoja (1) , panga jipya na ufagio wa chelewa.

**F: KIFUNGUA KINYWA NA CHAKULA CHA MCHANA KWA WANAFUNZI: KWA MWAKA 2021**

- Mahindi debe 04
- Maharage debe 01
- Chumvi pakti 02
- Mafuta ya kula lita 02 (lita mojamoja) **siyo ya kupima.**
- Fedha shilingi 30,000/=
- Sukari kilo 4
- Kikombe 1,Sahani 1 ,Kijiko 1

***NB: Ni lazima kwa wanafunzi wote kwa mujibu wa sheria***

G**: MAHITAJI MENGINE**

- Mwavuli wa kujikinga mvua
- Viatu vya matope (Gum boots)

**H: HOSTELI**

Shule inahosteli kwa wanafunzi wa kiume na wakike hosteli mahitaji ni kama yafuatayo:

**i. CHAKULA**

1. Maharage debe 3
2. Mahindi debe 10
3. Fedha Tsh. 150,000/=

**ii. MAVAZI**

**(a) WASICHANA**

1. Traki suti nyeusi
2. Gauni la bluu bahari (laiti bluu) kitambaa kizito la kuvaa kanisani.
3. Taulo
4. Blanket rangi yoyote.
5. Shuka mbili (2) rangi ya pinki
6. Ndoo moja (1) ya lita kumi na kidumu cha lita 5 cha kuhifadhia maji ya kunywa
7. Neti (chandarua) 1
8. Tranka (sanduku la bati) moja (1)
9. Godoro la Futi $2^{1/}2$ moja
10. Na mahitaji mengine kama vile sabuni, sahani,mswaki,mafuta ya kupaka,kikombe,kiwi, n.k.
11. Kadi ya Bima ya afya kwa wenye bima

**(b) WAVULANA**

1.Traki suti Light bluu
2. Suruali nyeusi.
3.Taulo

4.Blanket rangi yoyote.
5.Shuka mbili (2) za light bluu
6. Shati la bluu mikono mirefu
7. Ndoo moja (1) ya lita kumi na kidumu cha lita 5 cha kuhifadhia maji ya kunywa.
8. Neti(chandarua) 1
9. Tranka (sanduku la bati) moja (1)
10. Godoro la Futi $2^{1/}2$ moja
11. Na mahitaji mengine kama vile sabuni, sahani,mswaki,mafuta ya kupaka,kikombe,kiwi, n.k.
12. Kadi ya Bima ya afya kwa wenyenazo

***NB: Nguo za nyumbani haziruhusiwi kwa wanafunzi wa hosteli.***

# 03:SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
3. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
9. Kutunza mali za umma; na
10. Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki silaha ya aina yoyote ile.

### 3.1 Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa shule

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga

3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kusababisha mimba
9. Kuoa au kuolewa
10. Kutoa mimba/ kusababisha kutoa mimba.
11. Kugoma , kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na laini au simu ya mkononi.
14. Lugha chafu au ya kejeli kwa walimu na watumishi wengine, wazazi/walezi au wanafunzi wenzake.

**4.0. Hati za Lazima zinazopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi**

1. ***Medical Examination Form' ambayo itajazwa na Mganga wa Zahanati au Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni***
2. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai
3. Fomu ya uthibitisho wa mzazi na mwanafunzi
4. Nakala ya kitambulisho cha Uraia au Cheti cha kuzaliwa.

**5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ Maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**-----------------------------------------**

**MKUU WA SHULE**